# Haki Zako katika Utafiti

## Ukurasa wa Taarifa kwa Watu Wanaoshiriki katika Utafiti wa Uhamaji wa Kulazimishwa.

Kushiriki katika mradi huu wa utafiti unakupa nafasi ya kufanya sauti yako isikike, lakini pia unaweza kusababisha usumbufu, kugharimu muda au fedha/au kukufanya ujisikie vizuri kimwili na kiakili. Karatasi hii inaelezea maeneo muhimu na kuainisha haki zako.



### *Hiari, Idhini baada ya kueleweshwa*

Hii ina maana kwamba wewe ndio mwenye uamuzi wa kutaka au kutotaka kushiriki katika mradi huu wa utafiti.

Ngoja tuelezee hili kwa undani

**Hiari/Bila kulazimishwa** ina maana unaweza kuamua utakavyo–bila adhabu yoyote kwa kukataa kushiriki na bila mafao makubwa (kama kiwango kikubwa cha fedha) kwa kukubali kushiriki.

- Hautonyimwa bidhaa au huduma kwa kukataa kushiriki.
- Hata kama afisa wa serikali au shirika atapendekeza ushiriki katika utafiti, sio lazima ufanye hivyo. Utaendelea kuwa na haki ya huduma na rasilimali zile zile hata kama usiposhiriki.

**Umejulishwa/Fahamishwa** inamaanisha una haki ya kujua utafiti huu unahusu nini au wa kitu gani, unachoombwa kufanya na faida zinazoweza kupatikana na hatari ya kushiriki.

- Uliza utafiti utachukua muda gani na kipi haswa kinahitajika kutoka kwako.
- Una haki ya kujua jinsi utafiti utakavyoshirikisha watu/idara zingine na jinsi unavyoweza kuona majibu au matokeo ya utafiti.
- Una haki ya kupata taarifa katika lugha unayoielewa. Unaweza kuomba kupatiwa mkalimani au kutafsiriwa kama unahitaji.
- Mtafiti lazima akupe njia ya kuwasiliana naye ili endapo utakuwa na maswali au dukuduku. Njia hii ya mawasiliano inaweza pia kutumika endapo utataka kujitoa kwenye ushiriki wa utafiti hapo baadae.
- Una haki ya kuuliza maswali wakati wowote.

# Haki Zako katika Utafiti

**Ridhaa** inamaanisha umekubali bila kipingamizi chochote kushiriki.

- Hakuna anayeweza kutoa ridhaa kwa niaba yako (isipokuwa kwa walio na umri chini ya miaka 18 au watu wazima wenye uwezo mdogo wa utambuzi; tizama hapo chini juu ya idhini katika kesi za namna hii).
- Kwa kawaida, utaombwa kutia sahihi kwenye fomu kuashiria kwamba umeridhia kushiriki katika utafiti. Una haki ya kujadili na ndugu, marafiki, wafanyakazi wa makazi, wanajumuiya, au mtu yeyote mwingine kabla ya kuamua kutia sahihi au la.
- Endapo utapendelea, unaweza kuomba kutoa ridhaa kwa maneno badala ya maandishi. Wakati mwingine hili haliwezekani kutegemea na mahitaji ya mtafiti wa Bodi ya Maadili ya Utafiti–Research Ethics Board (REB).[1]
- Unaweza kujitoa kutoka kwenye utafiti wakati wowote–haulazimiki kumaliza utafiti. Endapo utaamua kujitoa, una haki ya kuomba taarifa zako zozote zisitumike.
- Pia unaweza kukataa kujibu swali lolote au kushiriki katika sehemu au eneo fulani la utafiti.

**Idhini** inamaanisha mtu mwenye umri wa chini ya miaka 18 au mwenye uwezo mdogo wa utambuzi amekubali kushiriki. Katika kesi kama hizi, mzazi au mlezi lazima atoe ruhusa ili utafiti uendelee. Kwa maneno mengine, inahitajika ridhaa na idhini.

---

[1] Bodi ya Maadili ya Utafiti–A Research Ethics Board (REB) ni kamati katika taasisi ya utafiti, ambayo ina jukumu la kupitia miradi ya utafiti kuhakikisha kwamba mtafiti wanazingatia kanuni za maadili zilizoelezewa katika nakala hii. REB itafanya kazi zake kukuza na kuzingatia haki zako katika utafiti.

# Haki Zako katika Utafiti



**Haki yako ya faragha na usiri** inamaanisha kwamba mtafiti hawezi kukutambua wewe au majibu yako katika utafiti bila ruhusa yako. Baadhi ya mambo ya kufikiria:

***Faragha*** **ni haki ya kutoingiliwa au kubughudhiwa na haki ya kuwa na mamlaka kudhibiti taarifa zinazokuhusu.**

- Una haki ya kuomba utafiti ufanyikie katika eneo la faragha na salama, ambapo watu wengine hawawezi kukutambua na kujua kwamba umeshiriki katika utafiti.
- Una haki ya kuchagua kama unataka kutambulika katika matokeo ya utafiti au la. Katika baadhi ya kesi, mtafiti hatoweza kutumia jina lake halisi, hata kama utamuomba, kwa sababu hiyo inaweza kuwatambulisha wengine katika utafiti ambao walichagua kutotambulika.
- Una haki ya kujua jinsi taarifa kutoka kwenye utafiti zitakavyotumiwa.
- Watafiti wanatakiwa kueleza kinagaubaga jinsi utakavyoweza kujua kuhusu matokeo ya utafiti.

***Usiri*** **ni ulinzi wa taarifa zako binafsi.**

- Mtafiti lazima awe na njia ya kutunza taarifa zinazokusanywa ili watu wengine wasiweze kuzipata.
- Una haki ya kujua ni kwa muda gani taarifa zako zitahifadhiwa na nani atakayekuwa na uwezo wa kuzipata.
- Mtafiti haruhusiwi kutoa au kuuza taarifa hizi kwa mtu mwingine asiyehusika.
- Katika baadhi ya kesi, mtafiti anaweza kuwa na jukumu la kimaadili kutoa taarifa juu ya nia ya kujidhuru mwenyewe au kudhuru wengine. Idhini inatakiwa ieleze waziwazi kuhusu mipaka ya usiri. Ikiwa una mashaka, uliza! Pia una haki ya kusisitiza juu ya usiri (tizama hapo chini) wa taarifa zozote zinazokusanywa kukuhusu.

# Haki Zako katika Utafiti

- Katika baadhi ya kesi, mtafiti anaweza kuwa na jukumu la kimaadili kutoa taarifa polisi juu ya vitendo vya kihalifu. Idhini inatakiwa ieleze waziwazi kuhusu mipaka ya usiri. Ikiwa una mashaka, uliza! Pia una haki ya kusisitiza juu ya usiri (tizama hapo chini) wa taarifa zozote zinazokusanywa kukuhusu.
- Unapojibu maswali ya kiutafiti kupitia mtandao, yakupasa kutambua kwamba taarifa zozote zinazokusanywa kwenye seva katika baadhi ya nchi kwa mfano Marekani, zinaweza kupitiwa na serikali. Una haki ya kuuliza jinsi ambavyo mtafiti atahakikisha usiri na faragha katika mazingira hayo.

***Kutojulikana*** **inamaanisha hakuna taarifa zinazoweza kukutambulisha, ili matokeo ya utafiti yakaweza kufuatiliwa na kuweza kukutambua.**

- Hili ni jawabu au suluhu moja katika mipaka ya usiri iliyojadiliwa hapo awali/juu: kwa kuhakikisha kwamba namna taarifa zinavyokusanywa hakuna mtu–hata mtafiti mwenyewe–anajua taarifa hizo zinamhusu nani.
- Kama hali yako ya uhamiaji haijaratibiwa, yakupasa uulize jinsi mtafiti atakavyohakikisha kwamba taarifa zako zinafanywa kuwa za siri. Kinyume cha hapo, matokeo ya utafiti yanaweza kukuweka katika hatari.



***Jukumu la mtafiti kutodhuru*** **inamaanisha kwamba ustawi wako, hadhi yako, na usalama wako unazingatiwa wakati wote.**

- Endapo katika wakati wowote ule wa utafiti unakuwa na wasiwasi au hujisikii kuendelea, una haki ya kumwambia mtafiti.
- Endapo mtafiti anaendelea kukufanya uwe na wasiwasi au shauku, mwambie mtu unayemuamini (rafiki,mwanafamilia, mfanyakazi wa makazi, mwanajumuiya) na uwasiliane na Bodi ya Maadili ya Utafiti au REB ya mtafiti. Njia za kuwasiliana nao zitakuwepo kwenye fomu ya idhini. Au unaweza kupata taarifa za jinsi ya kuwasiliana nao kupitia mtandao. Vyuo vikuu na hospitali zote zina REB au kamati inayofanana na Bodi ya Maadili ya Utafiti au REB.
- Una haki ya kutendewa kila kitu kwa heshima na hali ambayo inajali na kuzingatia utamaduni, dini na historia ya asili au kabila lako.